



JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



MATANGAZO: DOMINIKA YA 3 YA KWARESIMA A - TAREHE 08.03.2026

1.	LEO DOMINIKA 08.03.2026 DOMINIKA YA ZAKA	DOMINIKA YA 3 YA KWARESIMA MWAKA A Takaso la I la Wakatekumeni Mchango wa Pili ni kwa ajili ya Ujenzi
2.	IJUMAA 13.03.2026	Njia ya Msalaba saa 10:30 jioni ikiongozwa na UTOTO MTAKATIFU na itafuatiwa na Misa Takatifu. Kwa kipindi cha Kwaresma, siku za Ijumaa hakutakuwa na Misa za asubuhi. Matoleo kipindi cha Kwaresma ni kwa ajili ya Kampeni ya Kwaresma
3.	JUMAMOSI 14.03.2026	USAFI WA MAKABURI: Waamini wote wanaalikwa kufanya usafi katika makaburi ya kibaoni mara baada ya sala za Jumuiya kuanzia saa 3:00 asubuhi. Tuje na jembe, panga, fyekeo, reki, n.k. Jumuiya na Kanda zihamasishe waamini kushiriki kwa wingi.
4.	DOMINIKA 15.03.2026	DOMINIKA YA 4 YA KWARESIMA MWAKA A Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi Wasimamizi: Mt. Antoni wa Padua Watangaza Neno: Flora Bundala na Pancracia Shirima Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhu Wasimamizi: Mt. Augustino Watangaza Neno: Estha William na Yvoni Dominiki Misa ya 3: Saa 5:00 asubuhi Wasimamizi: Mt. Antoni wa Padua na Mt. Augustino Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi.
5.	VIWAWA	Jana 07.03.2026 kulikuwa na HIJA YA VIJANA JIMBO; jumla ya vijana 46 wa Parokia yetu walishiriki. Tunawapongeza kwa ushiriki wao.
6.	SEMINA YA VIJANA	Kutakuwa na Semina kwa vijana wote waliomaliza Kidato cha nne leo Dominika 08.03.2026 mara baada ya Misa ya kwanza Dondoo 1. Stadi za bustani na maisha 2. Kujenga tabia 3. Elimu ya afya na afya ya akili 4. Maandalizi ya kidato cha tano na chuo
7.	KUSALI KATIKA KANDA	Tutasali katika Kanda Jumamosi ya 21.03.2026 hivyo viongozi wa Kanda wanaombwa kutuma jina la mahali watakaposali (yaani jina la Jumuiya na jina la familia watakapokutana).

8.	MOYO MTAKATIFU WA YESU	Wanamoyo Mtakatifu wa Yesu watakuwa na kikao chao leo Dominika 08.03.2026 mara baada ya Misa ya Kwanza.
9.	KONGAMANO LA UTOTO MTAKATIFU TAIFA	Baraza la Maaskofu limeandaa Kongamano la Utoto Mtakatifu kitaifa jimboni Kigoma, 18-22 Juni, Kauli mbiu: Kujifunza, kujitambua – Utoto Mtakatifu na Umisionari. Gharama ya ushiriki kila mmoja Shs. 315,000/=. Mwisho wa kulipia ni tarehe 31.03.2026.
10.	HARAMBEE MAALUMU	Harambee maalumu kwa ajili ya kukamilisha ukumbi wa Parokia na rangi jengo la Kanisa ilifanyika 22.02.2026. Hata hivyo sio waamini wote waliweza kushiriki. Tunatoa nafasi kwa ajili ya waamini ambao hawakuweza kushiriki na wao kushiriki katika kuchangia. Unaweza kutoa ahadi yako kupitia viongozi wa Jumuiya yako au moja kwa moja kwa viongozi wa Kamati Tendaji Parokia. Kila Jumuiya inaombwa kuwasilisha taarifa kamili ya waamini/familia zilivyoahidi katika Harambee hii. Mwisho wa kumamilisha ahadi hizi ni 30.04.2026.
11.	UCHAGUZI WA KAMATI TENDAJI	Uchaguzi wa Kamati Tendaji Parokia ulifanyika Dominika iliyopita 01.03.2026 na viongozi wapya walichaguliwa watakaohudumu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa. Tunaalikwa kuwaombea na kuwapa ushirikiano ili waweze kutekeleza utume wao.
12.	MAHITAJI KWA WAHIJATI KIPINDI CHA PASAKA	Waamini wote wanaalikwa kutoa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya wahitaji kwa kipindi cha Pasaka ikiwa ni sehemu ya tulichojinyima kipindi hiki cha Kwaresima. Mahitaji ni kama nguo, chakula, sabuni, n.k. Vyakula vinavyoharibika kama nyama viletwe Parokiani siku ya Jumamosi Kuu 04.04.2026 saa 4:00 asubuhi. Vitu yote vikabidhiwe ofisini kwa karani na viorodheshwe kwenye daftari.
13.	WAWATA	Mafungo ya WaWATA Kiparokia yatafanyika hapa Parokiani katika Jumamosi ya tarehe 28.03.226 saa 3:00 asubuhi.
14.	HUDUMA YA MACHO	Kutakuwa na upimaji wa macho hapa Parokiani Dominika ya 22.03.2026 mara baada ya Misa ya kwanza mpaka saa 7:00 mchana. Huduma ya kupima 3,000 miwani kuanzia 15,000 na kuendelea.
15.	GAZETI LA TUMAINI LETU	Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5.

TANGAZO LA DARAJA YA UPADRI KWA MARA YA PILI

Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFM Cap wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anatangaza Daraja ya upadri wa Shemasi Peter Maksensius Mtendavema, SDS wa Shirika la Mungu Mwokozi - Wasalvatoriani (The Society of the Devine Savior) anayefanya uchungaji kwa sasa katika Parokia ya Mwenge katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam na anatarajia kupewa Daraja Takatifu ya Upadri tarehe 25.04.2026 katika Parokia ya Mwenge Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Tumuombee ili aweze kufikia Daraja hiyo anayoitamani.

MASOMO YA DOMINIKA

DOMINIKA YA 4 YA KWARESIMA MWAKA A - TAREHE 15.03.2026

SOMO I	1Sam.16: 1b, 6-7, 10-13a
WIMBO WA KATIKATI	Zab. 23
SOMO II	Efe.5: 8-14
SHANGILIO	Yn.8:12
INJILI	Yn.9: 1-41